

UHALISI WA MATABAKA KATIKA RIWAYA YA *VUTA N`KUVUTE*

Halima Badru Mohamed

halimabadru519@gmail.com

School of Swahili and Foreign Languages

Department of Swahili

Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA)

Received: April 2024 2024, Accepted June 2024, Published June 2024

© SUMAIT University Journal 2024

Abstract:

*This paper discusses the reality of classes in the *Vuta n`Kuvute* novel (1999). The research data was collected through critical reading and analysis in which the researcher read and critically analysed the novel along with different written materials which are not literary works of the topic. The selection of this novel was founded on the first information which the researcher came across on the reality of the history of Zanzibar. The data analysis was done by using Social Realism Theory. The findings generally reveal four types of classes found in the novel. These are political, economic, cultural and social classes. The study further shows that the writer of the novel was able to portray the reality of the classes that existed during the reign of the British rule because what he explained reflected the real situation of the life of that time.*

Ikisiri:

Makala hii inazungumzia uhalisi wa matabaka katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute* (1999). Data za utafiti uliofanyika zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji na uchambuzi makini wa maandiko. Mtafiti aliisoma na kuichambua kwa makini riwaya ya *Vuta n`Kuvute* pamoja na maandiko mbalimbali ambayo si ya kubuni yenye kuhusiana na mada. Kuteuliwa kwa riwaya hii kulitokana na taarifa za awali alizokuwa nazo mwandishi wa makala hii kuhusu uhalisi wa historia ya Zanzibar katika riwaya hii. Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa. Makala inafafanua aina nne za matabaka zilizobainika katika riwaya hiyo. Nazo ni; matabaka ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Aidha, uchanganuzi umeonesha kwamba, mwandishi wa riwaya hiyo amefanikiwa kuusawiri uhalisi wa matabaka katika jamii ya Zanzibar wakati wa utawala wa Uingereza, kwani; anayoyaeleza yanaakisi hali halisi ya maisha katika wakati huo ndani ya jamii husika.

Keywords: Uhalisi, Matabaka, Uhalisia Wa Kijamaa, Riwaya Ya *Vuta N`Kuvute*

1.0 Utangulizi

Uhalisi ni dhana inayotumiwa katika fasihi kuelezea hali ilivyo katika jamii kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni (Wamitila, 2003). Mtaalamu huyu anaendelea kueleza kuwa, uhalisi ni kaida muhimu katika dhana ya Ushabihikweli. Akifafanua dhana ya Ushabihikweli, Wamitila anaeleza kuwa, ni dhana inayotumiwa kurejelea hali inayofikia katika fasihi ambapo mwandishi huteuwa na kuwasilisha malighafi yake kwa jinsi inavyokaribiana na ukweli kama ulivyo katika maisha ya kawaida. Kutokana na maelezo hayo tunaweza kusema kuwa uhalisi ni ukweli. Wamitila (2008) anaeleza kuwa ukweli katika fasihi unaweza kuhusishwa na usahihi wa kihistoria unaoweza kufungamanishwa na kazi za kihalisia. Uhalisia unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu (Njogu na Wafula, 2007). Kwa kiasi kikubwa kazi ambazo zinaangaliwa kama za kihalisia, zinatarajiwa kuwa kama kioo cha hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika. Mulokozi (2017) anaweka wazi kuwa kazi za Adam Shafi ni miongoni mwazo.

Utabaka ni dhana inayorejelea mgawanyiko katika jamii kutokana na kubaguana kwa misingi ya kidini, kijinsia, kipato, kikabila, kielimu, rangi na hata mahali atokapo mtu (Sengo, 1987). Dhana ya matabaka inafafanuliwa vizuri na Marks na Engels (1845) kwa maelezo kuwa matabaka katika jamii hutokea pale ambapo baadhi ya wanajamii wanakuwa na kipato kikubwa zaidi kuliko wengine, hasa kutokana na unyonyaji unaofanywa na kundi lililo na uwezo wa mali katika jamii dhidi ya tabaka masikini. Uwepo wa matabaka ni jambo lisilopingika kutokana na historia ndefu ya binadamu hasa katika suala zima la uzalishaji mali (Rodney, 1973). Utabaka ulianza kutokea kulingana na mabadiliko ya mifumo ya uzalishaji katika jamii, ambayo ni ujima, utumwa, umwinyi, ubepari na ujamaa.

Kuhn (2004) anaeleza kwamba duniani utabaka ulianza kuibuka katika jamii za kale za wawindaji mnamo miaka 11000 iliyopita. Huko Ugiriki ya Kale na Roma, wakati wa utumwa, tabaka tawala lilijikita katika umilikaji wa uzalishaji wa watumwa, malighafi na zana za uzalishaji. Katika kipindi cha ubwanyenye huko Ulaya mabwanyenye walikuwa na mamlaka kwa wakulima. Katika kipindi cha umwinyi jamii zilijimarisha zaidi kijeshi na umiliki wa ardhi. Mfumo huu uliruhusu kuibuka kwa utabaka katika jamii. Edward (1997) anaeleza kuwa dhana ya utabaka ilianza kutumika Ulaya mnamo karne ya 18 pale muundo wa jamii ulipohusishwa na amri na cheo, utukufu uliongezeka kwa tabaka la juu, ndoa zilitumika kujiongeza utukufu. Edward anaweka wazi kuwa, matabaka yaliimarika zaidi karne ya 19 kuelekea ya 20. Hata hivyo, Almeida (2006) anaeleza kuwa katika nchi za Ulaya pengo lililopo kati ya tabaka la kati na la wafanyakazi ni dogo na linaendea kupungua. Sababu kuu ni mifumo imara ya mataifa yaliyoendelea.

Katika nchi za Afrika, wakati wa utawala wa Watemi jamii zilijengwa kitabaka (Rubanza, 1994) akinukuliwa na (Haji, 2018). Williams (2003) anaeleza kuwa katika jamii ya Watemi kulikuwa na tabaka la juu, kati na la chini. Anaendelea kueleza kuwa matabaka haya yalikuwa muhimu; kwani, yalizingatia hadhi na umaarufu. Katika Afrika Mashariki maeneo yaliyokaliwa na Wanyamwezi na Wasukuma wakati wa utawala wa Watemi yalikuwa na tabaka tawala na tabaka tawaliwa, ambapo tabaka tawala ndilo lililomiliki ardhi yenye rutuba. Wakati wa Utumwa na Umwinyi Zanzibar, jamii pia iligawika kimatabaka. Kulikuwa na tabaka lililomiliki ardhi na la watumwa. Baada ya kuingia Waarabu jamii iligawika matabaka matatu; Waarabu, Washirazi na Waafrika. Matabaka haya yalizingatia rangi na dini (*Institute of Education*, 1981). Kuanzia 1890 Zanzibar ilianza kuwa chini ya hifadhi ya Uingereza. Mwingereza alikuwa ni mkoloni mwenza wa Mwarabu (Davine, 1973; Speller, 2007). Folkers (2014) anaonesha kuwa utawala wa Uingereza uliimarisha utabaka katika

Zanzibar. Katika namna hiyo jamii iliongozwa kwa kuzingatia misingi ya ubaguzi wa rangi. Wamitila (2002:114) anafafanua kwamba uchunguzi wa riwaya unaambatana na uhalisi kwa kiasi kikubwa hivi kwamba haiwezekani kuzungumzia riwaya bila kurejelea mawazo yanayohusishwa na uhalisi. Hivyo, makala hii inachunguza namna riwaya ya *Vuta n'Kuvute* inavyowasilisha uhalisi wa matabaka katika Zanzibar wakati wa utawala wa Uingereza ili kubainisha uhalisi huo.

Tafiti mbalimbali zinaweka wazi kuwa Adam Shafi anaandika riwaya kwa kuzingatia matukio halisi ya kihistoria katika Zanzibar (Senkoro, 2011; Adam, 2014; Haji, 2015; Mbatiah, 2016; Mulokozi, 2017; Gathanya, 2018). Tafiti hizo zinaishia kutaja tu kuwa Adam Shafi anaandika riwaya kwa kujiegemeza katika historia halisi ya Zanzibar, bila ya kufafanua matukio hayo kwa kina. Vilevile, tafiti hizo hazijahusisha uwanja wa fasihi na uhalisi wa historia ya Zanzibar. Kwa mantiki hiyo, jitihada za kutosha hazijafanywa kuuchunguza uhalisi wa matukio ya kihistoria yanayosawiriwa na mwandishi husika katika riwaya teule. Kwa maoni ya mtafiti, kutofanyika kwa utafiti zaidi kuhusu uhalisi wa matabaka yanayosawiriwa katika riwaya ya *Vuta n'Kuvute*, kunadumaza mawanda ya kuelewa mwingiliano taaluma uliyopo baina fasihi na historia katika riwaya teule. Aidha, ni kikwazo kwa jamii kuelewa namna riwaya hiyo inavyoweza kutumika katika kujifunza historia halisi ya Zanzibar.

Ufafanuzi huu unalenga kutoa dira kuwa fasihi ni zao la jamii na kwa kiasi kikubwa ni historia kama anavyofafanua Mapara (2007). Aidha, ni kuonesha kuwa fasihi ina ukaribu mno na uhalisi katika jamii. Pamoja na kudhihirisha ukweli kuwa riwaya zinawakilisha mifumo ya kijamii ikiwamo ya kiutawala, kiuchumi na kiutamaduni katika jamii maalumu. Kwa kuwa uhalisi ni ukweli, basi ukweli huu katika fasihi unaweza kuhusishwa na usahihi wa kihistoria kama ambavyo inaelezwa na Wamitila (2008). Waandishi wa kazi za fasihi hujikuta wakikumbwa na kaida ya kuchota historia katika kuziandika kazi zao. Njogu na Chimera (1999) wanafafanua kuwa msanii hujaribu kuwasilisha matukio ya kijamii katika uhalisia wake. Msanii huchota maudhui yake kutokana na hali halisi za kiuchumi, kiutamaduni, kijamii na kisiasa katika mazingira yanayomzunguka. Hivyo ndivyo alivyofanya Adam Shafi katika riwaya ya *Vuta n'Kuvute* (1999) kwa kuegemea historia ya Zanzibar wakati wa utawala wa Uingereza. Hivyo, kitendo cha mwandishi kuisawiri historia kilimsukuma mwandishi wa makala hii kubaini namna fasihi inavyoweza kuwa hazina ya kujifunza historia halisi ya Zanzibar kuhusu suala la matabaka wakati wa ukoloni. Kwa mantiki hiyo, makala hii imechunguza uhalisi wa matabaka ndani ya Zanzibar katika riwaya ya *Vuta n'Kuvute*.

2.0 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti uliozaa makala hii uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaakatika mchakato wote wa ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wake. Uhalisia wa Kijamaa ni mbinu ya utunzi na uhakiki inayomzingatia binadamu kama uti wa mgongo wa kuwapo kwa ulimwengu na maana ya ulimwengu (Njogu na Wafula, 2007). Nadharia hii husisitiza kuwa mahusiano ya kiuchumi, kitamaduni na mifumo yote ya kijamii hutegemea mahusiano ya kiuchumi. Mulokozi (2017) anafafanua kuwa Wahalisia wa Kijamaa huonesha wahusika namna wanavyopambana dhidi ya mifumo kandamizi ya kijamii ili kujenga mifumo mipya isiyokandamizi. Fasihi hiyo huonesha migogoro ya kitabaka, hali ya wanawake na mapambano yao sambamba na wanaume katika kujitafutia hali bora zaidi.

Uchunguzi wa makala hii umejiegemeza zaidi katika muhimili wa binadamu kuoneshwa kiuyakinifu. Muhimili huu unaeleza kuwa binadamu huoneshwa kiuyakinifu. Wahusika ambao hutumiwa kama vipaza-sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao. Muhimili huu umetusaidia kuchambua uhalisi wa matabaka ndani ya Zanzibar unaosawiriwa katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute* kwa kuona namna matabaka ndani ya Zanzibar yanavyosawiriwa katika riwaya iliyotafitiwa. Tukio hilo limechambuliwa kwa mwegamo wa kifasihi kwa sababu, fasihi husawiri uhalisi katika jamii; kwani, mwanafasihi huandika vitu ambavyo tayari vipo na halisi (Senkoro, 1995). Kavoi (2020) anabainisha kuwa miongoni mwa masuala yanayozungumzwa katika riwaya za Zanzibar ni suala la misugvano ya tofauti baina ya matabaka mbalimbali katika jamii hiyo kabla ya uhuru. Ufafanuzi huu unayakinisha kuwa, fasihi ni zao la jamii. Kwa hivyo, suala la matabaka ndani ya Zanzibar linalojadiliwa katika makala hii ni lile linalosawiriwa katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute*. Suala hilo linatuwezesha kupata picha juu ya uhalisi wa matabaka ndani ya jamii ya Zanzibar wakati wa ukoloni. Hivyo, *Vuta n`Kuvute* ni zao la jamii inayoonesha kuwapo kwa jamii hiyo kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.

3.0 Methodolojia

Makala hii ilitumia mkabala wa kitaamuli katika ukusanyaji, uchanganuzi na utoaji wa matokeo ya utafiti uliofanyika. Mkabala wa kitaamuli kwa kawaida hautoi kipaumbele katika masuala ya takwimu, unahitaji zaidi ufafanuzi na maelezo (Enon, 1998; Ponera, 2019). Ponera (2019) anaongeza kuwa data katika utafiti wa kitaamuli hupambanua jambo kwa kina na kuonesha ukweli wa jambo. Aidha, anafanua kwamba utafiti wa aina hii hulenga kugundua maana ya matukio yaliyowakumba watu na namna yalivyowaathiri. Hivyo, mkabala huu umetumika kwa sababu utafiti uliofanyika umechambua maandishi ya kifasihi yanayofungamana na muktadha wa kihistoria katika jamii ya Zanzibar kwa kuchanganuliwa, na kufafanuliwa kwa njia ya maelezo.

Data za utafiti uliozaa makala haya zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji na uchambuzi makini wa maandiko. Mtafiti aliisoma na kuichambua kwa makini riwaya ya *Vuta n`Kuvute*. Mtafiti alifanya hivyo ili kupata data za msingi ambazo zilihitaika kulingana na lengo la makala hii. Katika hali hiyo, mtafiti aliweza kubainisha data za uhalisi wa matabaka ndani ya Zanzibar unaosawiriwa katika riwaya teule. Kwa msingi huo, data zilizopatikana kutokana na usomaji na uchambuzi makini wa maandiko zilikuwa mahususi kwa kupima lengo hilo.

4.0 Uhalisi wa Matabaka Katika Riwaya ya *Vuta n`Kuvute*

Kiini cha riwaya hii ni suala la mvutano uliopo baina ya watawala na watawaliwa, pia baina ya wazazi na watoto katika suala la mapenzi. Suala la matabaka linasawiriwa vyema kupitia riwaya hii. Hivyo, riwaya hii inahusu mabadiliko katika jamii, watu kudai haki zao. Aina hii ya riwaya imekusudia kuleta usawa na haki katika jamii. Aidha, *Vuta n`Kuvute* ina lengo la kujenga jamii mpya isiyo na matabaka. Jamii iliyojikomboa katika nyanja zote za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kifikra. Jamii isiyo na unyonyaji wa aina yoyote, jamii ambayo hatamu za uongozi zingekua mikononi mwa wafanyakazi na wakulima. Utafiti uliozaa makala hii ulibaini kwamba wakati wa utawala wa Uingereza ndani ya Zanzibar jamii iliishi kimatabaka. Hali hiyo ilisababishwa na mfumo wa maisha katika jamii hiyo uliowakweza watu weupe na kuwatweza weusi. Makala hii inabainisha uhalisi wa matabaka katika riwaya hiyo kama ifuatavyo:

4.1 Uhalisi wa Matabaka ya Kisiasa

Katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute* mwandishi anasawiri matabaka ya kisiasa kwa namna ambayo kuna tabaka tawala na tawaliwa. Tabaka tawala ni la Waingereza linawakilishwa na Kamishna, na Inspekta

Wright, waliheshimiwa na ndio watawala wakuu. Kuna Waarabu ambapo Sultani ametajwa kuwa ni kiongozi anayeongoza kwa matakwa ya Uingereza. Sultani anataka kuuliwa na wanaharakati wanaodai uhuru. Tabaka tawaliwa ni la Wahindi na Waafrika. Wahindi wanawakilishwa na Bwana Raza, Kermali, Gulamu, Mama Yasmin na Yasmin. Waafrika wanawakilishwa na Denge, Mambo, Mwajuma, Chande, Hanifa, Kijumbamshare na Mabalanga. Waafrika ndilo kundi linalopinga kutawaliwa. Dondoo lifuatalo linathibitisha kuwapo kwa tabaka tawala na tawaliwa:

... watu ambao walikuwa wengi, wengine walikuwa wakiranda bila ya kazi... Kwa vile Serikali ya Bwana Sayyid chini ya himaya ya Muingereza haitambui elimu ya nchi za kikoministi (uk.73).

Tunapoangalia dondoo hapo juu, muktadha wa maelezo umejengeka kitabaka. Maelezo yanatuonesha kwamba serikali inaendeshwa na Waarabu na Wazungu. Uongozi wa serikali hiyo ulikuwa ni wa kibaguzi, ulibagua watu kutokana na misingi ya rangi na itikadi. Mapuri (1996) anaonesha kuwa jamii ya Zanzibar wakati wa ukoloni iligawika katika matabaka. Tabaka la juu kabisa ni la Waingereza. Hawa ndio watawala wakuu katika Zanzibar. Tabaka linalofuatia ni la Waarabu. Wakiwamo Washihiri kutoka Yemen, na Wamanga kutoka Oman. Waarabu wa kabila la Al-Busaidy kutoka Oman ndio waliokuwa familia ya kifalme. Hawa walikuwa na nguvu za kisiasa na uongozi, walishirikiana na Waingereza katika shughuli za utawala. Washihiri walikuwa wakiendesha biashara maduka yao yalikuwa ya rejareja. Tabaka la tatu ni jamii ya Wahindi ambao pia walikuwa na hadhi na uwezo kijamii. Hawa walikuwa ni wafanyabiashara wakubwa na matajiri waliomiliki biashara za ndani na nje. Walipewa nafasi ya ushauri katika serikali juu ya masuala ya uchumi na walikuwa na nguvu katika sekta ya fedha. Tabaka la chini kabisa ni la wanaokandamizwa wengi wao ni Waafrika. Wengi kati ya hawa ni masikini wasio na ardhi. Wenye kukidhi maisha yao kwa kufanyakazi katika mashamba ya Waarabu, au kufanya kazi za ndani katika nyumba za Waarabu na Wahindi walio matajiri. Kazi nyingine zilizowawezesha Waafrika wa Zanzibar kuendesha maisha yao ni zile zenye malipo ya chini. Waafrika hawakuwa na dhamana yoyote katika kusimamia masuala ya nchi yao. Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa jamii ilikuwa katika matabaka. Loimeier (2018) anafafanua kwamba Waingereza, Waarabu, na Wahindi waliwaona Waafrika/Waswahili kuwa ni watu duni.

Uhalisi wa matabaka ya kisiasa katika *Vuta n'Kuvute* pia unabainika kupitia utawala wa Kiingereza namna ulivyowabagua wale waliopata elimu katika nchi za kikomunisti. Adam Shafi anasawiri hali inayoonesha kijana Denge anakosa ajira kwa sababu amesoma katika nchi hizo. Huyu amemaliza elimu ya Chuo Kikuu na amepata Shahada ya Ubingwa katika Fani ya Uchumi kutoka Urusi. Wakoloni walikuwa wanachukia ukomunisti kwa sababu ya shabaha za ukoloni na ukomunisti hazifanani. Batholomayo (2019) anaonesha kuwa ukomunisti hulenga kuifikisha jamii katika hali isiyokuwa na matabaka, ukoloni unaazimia kuwatawala watu kwa kuwatumikisha ili kujivunia faida kubwa iwezekanavyo. Hivyo, Serikali ya Kikoloni iliwabagua wote waliowahi kufika ama kupata elimu katika nchi za kikomunisti Denge akiwa ni mmoja wao. Mwandishi anaeleza:

Sasa ndio hawataki kukupa kazi? Sukutua alimwuliza Denge kwa huruma ... Nakwambia tokea siku niliyoshuka uwanja wa ndege wakaona pasipoti yangu kwamba n`natoka Urusi basi askari kanzu haweshi kunifuata na kuniuliza maswali (uk. 52).

Maelezo hayo yanathibitisha kuwa Denge anakosa ajira mbali na utaalamu alionao. Wakati wa ukoloni Urusi ilikuwa ni miongoni mwa nchi zinazopinga ukoloni. Hivyo, waliosoma katika nchi hizo hawapewi ajira katika Serikali ya Kikoloni. Wilson (2007) anafafanua kuwa baadhi ya vijana wa Zanzibar walipata elimu zao za Chuo Kikuu katika nchi za Kikomunisti Urusi ikiwamo. Mbali na masomo walivyoyaendea huko walipewa mafunzo ya siasa. Walifunzwa itikadi za Kijamaa ikiwa ni pamoja na kukataa kutawaliwa ambayo inakwenda kinyume na itikadi za kibepari. Wilson anaendelea kufafanua kuwa Abdul Rahman Babu ni mmoja wa Wazanzibari waliopata mafunzo ya itikadi ya kijamaa katika moja ya jumuiya za Kikomunisti huko Uingereza, *Communist Party of Great Britain* (CPGB). Aliporudi Zanzibar alionekana ni tishio kwa mipango ya Serikali ya Kiingereza. Wilson anaeleza kuwa Babu aliwahi kufungwa kutokana na shughuli hizo za kisiasa. Hii ni miongoni mwa mbinu iliyotumiwa na Serikali ya Kiingereza Zanzibar kuwatenga wanaharakati wa ukombozi. Naye Sheriff (2001) anafafanua kuwa Serikali ya Kiingereza iliweka sheria kwamba wajiriwa wote lazima wasijishughulishe na siasa. Kwa sababu Denge ni mmoja kati ya wanaotiliwa mashaka kuwa ni miongoni mwa wanaopinga kutawaliwa, moja kwa moja sheria hii inamkamata. Hivyo, ni wazi hana nafasi ya ajira katika serikali hiyo. Denge alitwa komunisti na alikuwa anafuatiliwa nyendo zake na serikali kwa kuwatumia watu wake wa karibu.

Tunaporejela muhimili wa Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa unaoeleza kuwa binadamu huoneshwa kiuyakinifu. Wahusika ambao hutumiwa kama vipaza-sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao (Njogu na Wafula, 2007, uk. 68). Muhimili huu umeakisi kwa kumuonesha binadamu katika uyaakinifu wake, tunaona jinsi riwaya inavyochora wahusika kama binadamu walio katika maisha halisi ya wakati wa ukoloni; kwani, matabaka ambayo mtafiti ameyabaini katika kazi ambazo si za kiubunifu kama vile Mapuri (1996), Sheriff (2001) na Wilson (2007) yanasawiriwa vyema katika riwaya teule. Hivyo, tunapata sura halisi ya jamii ya Zanzibar ilivyokuwa wakati wa ukoloni kupitia riwaya hiyo. Kwa jumla, kisiasa tunaweza kueleza kwamba wakati wa ukoloni jamii iligawika katika sehemu mbili kuu. Nazo ni tabaka tawala na la watawaliwa. Riwaya ya *Vuta n`Kuvute* inayasawiri matabaka haya kwa namna ambayo inaonekana wazi kuwa Waafrika hawakuwa na nafasi katika masuala ya kuiongoza nchi kama ambavyo inaonekana katika maandiko ambayo si ya kubuni.

4.2 Uhalisi wa Matabaka ya Kiuchumi

Katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute* matabaka ya kiuchumi yanasawiriwa kwa kuonesha kuwa katika jamii kuna tabaka la matajiri na masikini. Wenye nacho wanawakilishwa na akina Bwana Bashiri, Kermali na Gulamu. Mwandishi anasawiri makaazi ya Kermali kwa kueleza:

Nyumba yao ilikuwa ni ya kiroshani cha ghorofa moja, chini ndipo ilipo mitambo ya kutengezea "kulfi" ... Juu kuna ukumbi mdogo na vyumba viwili. Ukumbini pamepambwa kwa picha na makochi ya pale yalikuwa yale ya kubonyea (kur. 249 - 250).

Katika dondoo hilo Kermali amechorwa kuwa ni mtu mwenye nacho kutokana na makazi yake. Anaishi katika nyumba ya roshani, anamiliki mitambo, samani na mapambo ya kifahari nyumbani mwake. Hivi vyote ni vibainishi vya hali ya utajiri. Aidha, maelezo tunayoyapata katika (uk. 248) unazidi kutupa picha juu ya utajiri wa Kermali. Huyu ni mtu wa jamii ya Wahindi, ambaye anajishughulisha na biashara anamiliki duka kubwa la baiskeli. Katika hali ya kawaida masikini hawezi kuwa na umiliki wa vitu kama hivyo. Zanzibar kipindi cha ukoloni Wahindi ndio waliokuwa wafanyabiashara wakuu (Mapuri, 1996; Bakari, 2011; Sheriff, 2001; Loimeier, 2018).

Tunapojumuisha mawazo katika dondoo la hapo juu na yale tunayoyapitia katika kurasa za 1 na 2, katika riwaya inayotafitiwa tunaona bayana Adam Shafi anavyosawiri uhalisi anaeleza:

Kama desturi ya Wahindi wengi Afrika Mashariki, Bwana Raza alikuwa mfanyabiashara mashuhuri pale Mtendeni. Alikuwa na duka kubwa la reja reja pale (kur.1 - 2).

Dondoo linaonesha kawaida ya Wahindi wengi ni wafanyabiashara kama ambavyo tumeona katika kazi ambazo si za kubuni. Wahindi walijihusisha katika biashara zote za ndani na za nje. Aidha, utamaduni huo bado unaendelea kwa jamii hiyo. Hata hivyo, baada ya ukoloni wasiokuwa jamii ya Wahindi ndani ya Zanzibar nao wamekuwa wafanyabiashara wakubwa. Hii ni nafasi adhimu waliyoipata Waafrika wa Zanzibar baada ya safari ndefu ya msako wa uhuru katika nchi hiyo. Wakati wa ukoloni nafasi hii haikupatikana kwa Waafrika walio wengi kutokana na sera za kibaguzi zilizotamalaki katika jamii.

Aidha, Adam Shafi anaonesha matabaka ya kiuchumi kwa watu masikini katika namna anavyoisawiri nyumba ya Matar:

Ukiingia unakabilia na matalasimu yaliyojaa mabuibui yanayoning`inia darini. Ndani humo mnanyekenya kwa unyevunyevu wa ile nyumba kwa kukosa joto la binadamu. Harufu ya unyevunyevu ule inapalia kama vumbi kali kwa mtu asiyeizowea ... Ukumbi hauna sakafu, ni dongo tu nalo limeshiba unyevu wa nyumba ile. Pembeni kuna mtungi wa maji aliouweka juu ya sanduku tupu la mbao alilolikata katikati ili tako la mtungi ule likae vizuri juu yake ... Hapo pana viti viwili tu vya msonobari, vya zamani. Kuna bao refu limeshikamana na ukuta na bao hilo halina miguu. Miguu yake ni ya mawe makubwa moja upande huu na jingine upande ule. Madirisha ya hapo ni mawili ya mbao nne nne za kufungia, mbili juu mbili chini. Linalofunguliwa hapo ni dirisha moja tu nalo hufunguliwa zile mbao mbili za juu... Kwa sababu hiyo ukumbini hapo hapakuwa na mwanga wa kutosha (kur. 257 - 158).

Mandhari hayo yanawakilisha umasikini. Aidha, mbali na umasikini mwandishi pia anatuelekeza kuwa ni nyumba inayoonekana kukosa matunzo. Suala la usafi katika nyumba hiyo linaonekana ni la tabu. Mwandishi anapoeleza kuwa nyumba hiyo ilikosa joto la binadamu inamaanisha kuwa Matar alikuwa akiishi peke yake hana hata mke. Anapotoka kwenda na shughuli zake nyumba inabaki tupu. Mtafiti anaona kwamba umasikini wa Matar ndio unaomchangia kutofikiria suala la kuwa na mke; kwani, mke angehitaji huduma ambazo yeye hazimudu. Maelezo tunayoyapata katika dondoo hilo yanatuhakikishia kuwa Matar hakuwa na habari kabisa ya utunzaji wa mazingira katika nyumba yake. Emhemmd (2017, uk. 23) anafafanua kuwa mtu wa kwanza kuwajibika na usafi wa mazingira ni yule mtu anayeishi katika mazingira husika. Mtaalamu huyo anaonesha kuwa usafi una nafasi kubwa ya kuiepusha jamii kutokana na maradhi. Hivyo, Matar anaonekana si mtu aliyekuwa anajali afya yake kwa sababu usafi wa mazingira anayoishi hakuupa nafasi. Hali hii pia inaweza kuwa inatokana na sehemu kubwa ya watu kwa wakati huo hawakuwa na elimu juu ya chanzo cha maradhi tofauti.

Matabaka ya kiuchumi katika *Vuta n`Kuvute* hayajabainishwa kupitia makaazi tu bali hata kwa upatikanaji wa chakula. Kwa mfano mwandishi anaeleza:

Nyumbani kulikuwa kumeandaliwa vilivyo. Tambi za samawi, zilizotupiwatupiwa zabibu, mkate wa mayai, kaimati zilizoshurubu shira vizuri, mikate ya ufuta, mkate wa kumimina, changu mzima wa kupaka, chai nzito ya maziwa iliyokoleya iliki (uk 79).

Maelezo ya dondoo hapo juu yanaonesha kuwa fedha ipo. Maandalizi ya vyakula aina kwa aina masikini havimudu. Kwa masikini, aina mbalimbali za vyakula hivi vingeliliwa siku kadha si kwa siku moja hata kama amepata mgeni wa aina gani. Haya yanatokea kwa sababu kitu kipo afadhali. Vyakula hivyo vinaonesha utamaduni wa vyakula vya Zanzibar. Aidha, usanifu wa unga wa ngao unajitokeza.

Ingawa karamu hiyo ilijumuisha vyakula mbalimbali hata hivyo, haikuzingatia aina tofauti ya virutubisho. Mboga na matunda vimekosekana ili kutimiza mlo kamili. Kwa jamii, muhimu sana kupangilia mlo ili kuhakikisha tunapata virutubisho vyote tunapoandaa vyakula. Hii itatujengea siha njema na kutuepusha na tatizo la ukosefu wa afya njema. Katika jamii tunakabiliwa na tatizo kubwa la maradhi ya gesi. Kwa kiasi kikubwa tatizo hili linasababishwa na ulaji wa vyakula vyenye wanga zaidi kuliko aina nyingine. Aidha, unywaji wa maji ni suala la kulipa umuhimu pia. Tukinywa maji kwa kiasi kinachohitajika tutakuwa tunajijengea siha njema.

Tabaka masikini kupitia ulaji katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute* unaonekana kupitia dondoo lifuatalo:
*Alipohakikisha kuwa Mwajuma amemnunua yule samaki, alipumua na kuendelea kusinzia
kwa furaha kwani muda wa siku mbili jikoni mwao mlilala paka (kur.57 - 58).*

Mfano huo unabainisha hali ya umasikini wa Mwajuma. Kauli ya “jikoni mlilala paka” ina maana kwamba hamjapikwa. Hali hii inaonesha uduni wa upatikanaji wa chakula katika nyumba hiyo. Maelezo ya dondoo yanathibitisha kuwa hamkupikwa kwa kukosekana cha kupikwa; kwani, usinziaji wa furaha baada ya kuhakikisha kumenunuliwa samaki katika dondoo hilo kunaashiria ujengaji wa matumaini ya kula kwa anayesinzia. Hii inamaanisha kuwa njaa inamtafuna na kuwa alikuwa na mawazo moyoni juu ya upatikanaji wa chakula. Hivyo, samaki aliyenunuliwa alimjengea matumaini ya kupatikana cha kuliwa nyumbani mwao. Kwa kawaida mwenye nacho hakai hata siku moja asipikie seuze siku mbili.

Katika dondoo lingine mwandishi anaeleza:

*Hebu lete shilingi tano. ... Kukwambia kweli, Denge alisita na kuinamia chini, tokea chai
ya asubuhi kama nimeuma kitu ... (uk. 52).*

Maelezo ya hapo juu yanaonesha umasikini. Mtu kushindia chai tu iliyonywewa asubuhi kutwa nzima hajauma kitu ni ishara ya ukosefu wa fedha. Ingawa kuna watu huweza kufanya hivyo kutokana na harakati zao. Hata hivyo, kwa mujibu wa dondoo hali hiyo kwa Denge imesababishwa na ukosefu wa fedha. Denge na Mwajuma wanawakilisha tabaka la wasio nacho katika Zanzibar wakati wa ukoloni. Ukosefu wa kupata chakula kwa wakati unatubainishia umasikini wa watu hao.

Kwa jumla, kiuchumi jamii iligawika katika sehemu mbili kuu. Nazo ni tabaka la matajiri na masikini. Riwaya teule inasawiri matabaka haya kwa namna ambayo inaonekana wazi kuwa Waafrika wengi ndio waliokuwa masikini. Muhimili wa Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa kwa mujibu wa Njogu na Wafula (2007, uk. 68) unaoeleza kuwa binadamu huoneshwa kiuyakinifu. Wahusika ambao hutumiwa kama vipaza-sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao umetuongoza katika kubaini namna Adam Shafi anavyosawiri uhalisi huo wa kihistoria katika riwaya teule, kwani; matabaka tuliyoyabaini katika kazi zisizokuwa za kiubunifu kama vile (A.S.P, 1977; Khatib, 1992; Mapuri, 1996; Sheriff, 2001; Bakari, 2011; Loimeier, 2018) yanasawiriwa vyema katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute*.

4.3 Uhalisi wa Matabaka ya Kiutamaduni

Matabaka ya kiutamaduni katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute* yanabainika kwa namna ambayo mwandishi anaonesha kuna ubaguzi baina ya jamii ya Wahindi na Waswahili. Hali ya Wahindi kujitenga na Waswahili inaelezwa na Burton (2013). Mtaalamu huyo anafafanua kwamba Wahindi wanapenda kujiweka mbali na Waswahili. Kama tulivyotangulia kueleza hapo awali kuwa Wahindi katika Zanzibar wakati wa ukoloni walikuwa na hadhi zaidi wakilinganishwa na Waafrika mbele ya watawala. Hivyo, hadhi walivyokuwa nayo tunaweza kueleza pia ilichangia kwa kiasi kikubwa kujiona bora na hawafai kuchanganyika na Waswahili. Hali hii inadhihirika kupitia ndoa na mahusiano ya kawaida. Ravji (2013) akinukuliwa na Adam (2014: 75 - 76) anaeleza kuwa:

Kwangu mimi naona kuwa Mswahili ni mwanadamu na anastahili kupata heshima zote za kibinadamu. Lakini mimi nina utamaduni wangu na yeye ana utamaduni wake (Adam, 2014).

Mawazo yanayowasilishwa na dondoo hilo yanaelekea kutumiwa na jamii ya Wahindi kuhlalisha matabaka baina ya jamii mbili hizi. Maelezo ya mzungumzaji kuhusu utamaduni wangu na wake ni kauli ya kuweka mipaka. Wahindi wanatawaliwa sana na suala la utabaka ndio maana hawaishii kujitenga na Waswahili tu, bali hata ndani ya jamii yao utengano upo (Wahabi, 2022).

Katika masuala ya ndoa mwandishi wa riwaya ya *Vuta n`Kuvute* anaonesha Wahindi hupendelea kuozeshana wenyewe kwa wenyewe. Keshodkar (2010: 228) anaonesha kuwa Wahindi walipoanza kuhamia Afrika Mashariki walikuwa wakitaka kuoa huenda India na kurudi na wake wao wa Kihindi. Baadaye, jamii ilipoongezeka watoto wa kike waliozwa waume wa jamii zao. Adam Shafi katika kuisawiri hali hii anaeleza:

Mara tu baada ya kuvunja ungo, Yasmin aliozwa mume. Alikuwa mume wa jamii yake ya Ithinashiria ... Alikuwa ni mume asiyelingana naye hata kidogo. ... wakati Yasmin ni kigoli wa miaka kumi na tano tu, mumewe Bwana Raza alikuwa zee la miaka hamsini na mbili (uk.1).

Hali ya Yasmin kuozwa mume huyo ni katika kuimarisha utabaka. Wahindi hawazingatii muonekano wa mtu bali wanajali tabaka. Mawazo tunayoyapata katika dondoo hilo yanathibitisha kauli ya Keshodkar (2010) hapo juu. Maelezo ya dondoo pia tukiunganisha na maelezo yanayofuatia katika riwaya husika uk. 1. Yanafafanua wazi kuwa ndoa hiyo ilikuwa ya kupangwa. Rustamkhanli (2016) anaeleza kuwa ndoa za kupangwa kwa Wahindi ilikuwa ni jambo la kawaida. Mtoto wa kike hakuwa na nafasi ya kuchagua mume wazee ndio wanaoamua. Hivyo, hali hiyo inajitokeza katika haja ya kukuza utabaka kuinga kuchanganyika na jamii nyingine.

Wahindi huwa wagumu kuchanganyika na Waswahili katika mahusiano ya ndoa. Adam Shafi anaeleza:

Mwambie itapelekwa posa. ... Oh! Oh! Barka! aliruka Kermali ... Sasa Yasmin Bai unafikiri Gulam atakubali posa ya Mswahili? (uk. 251).

Dondoo hilo hapo juu linaonesha muktadha wa mazungumzo ya utabaka. Mzungumzaji anaposhangilia kwa kusema Oh! Barka! Anamaanisha habari ya posa ni jambo la heri yaani lenye kuleta utulivu. Hata hivyo, anahoji juu ya uwezekano wa kukubalika posa ya Mswahili kwa sababu ya ule utabaka waliojijengea. Ndoa inatazamiwa kuwa ni jambo la mafanikio. Khatib (1992: 35) anaeleza kuwa katika maendeleo ya binadamu ndoa ni kitu cha lazima. Anaendelea kufafanua

kwamba ni lazima kwa sababu ya faraja ya wapenzi wawili, kumwendeleza na kumrudufisha mwanadamu katika eneo kubwa la dunia linalohitaji wakaazi na wageuzaji wa maumbile kwa ajili ya aushi ya mwanadamu. Hivyo, mfumo wa ndoa za kitabaka hazina nafasi katika dunia ya sasa; kwani, ndoa ni maridhiano baina ya watu wawili wanaotegemewa kwenda kuanzisha maisha yao.

Diegner (2011) anaeleza mtazamo wa Adam Shafi juu ya ndoa kati ya Waswahili na Wahindi. Anafafanua kwamba ndoa baina ya Wahindi na Waswahili sio kama hazipo kabisa zipo isipokuwa ni za kutafuta sana. Anaendea kufafanua kuwa Mhindi kufunga ndoa na Mwafrika si tatizo, lakini Mhindi kuolewa na Mwafrika hiyo ngumu. Ugumu unakuja kwa sababu kufanya hivyo kwa mtoto wa kike ni kama kuidhalilisha jamii nzima ya Wahindi. Hali hii inathibitishwa na Keshodkar (2010) anapoeleza kwamba bi Fatima kutoka jamii ya Wahindi anaeleza kuwa ameamua asiolewe maisha kuliko kuolewa na Mwafrika. Hivyo, Adam Shafi anapoonsha kuhoji kwa Kermali kuhusu kukubalika posa ya Mswahili kwa Gulamu juu ya Yasmin anausawiri uhalisi wa jamii hiyo. Aidha, Adam Shafi anatufahamisha kuwa Gulam ana mke wa pili ambaye ni Mswahili anaeleza:

Unaona sasa? Kitu gani? aliuliza Kulsum. Sasa Yasmin anafuata nyayo. Yeye Gulamu mwenyewe ana mke wa Kiswahili na Yasmin naye anataka kuolewa na Mswahili. Gulam? Mke Mswahili? aliuliza Kulsum ameshangaa. Anaye mke Mswahili! ... Amemwoa kwa siri. Mke wake anajua ... hiyo siri imebakia nyumabni mwao tu. Haitoki nje (uk. 252)

Dondoo linaonesha Kulsum anashangaa kuwa Gulamu ana mke Mswahili. Kwa sababu kwao wao kuchanganyika na Mswahili ni kituko; kwani, halingani na wao. Hali ya Wahindi kuwa na wake Waswahili inathibitishwa na Wahabi (2022) anapoeleza kuwa Wahindi wanaume baadhi walikuwa wanaoa wake Waafrika. Mke huyu anaweza kuwa mke mkubwa au mdogo. Hata hivyo, mtaalamu huyo anaeleza kuwa watoto wanaopatikana na mke Mwafrika huwa hawathaminiwi katika jamii ya Wahindi. Kama ikitokea baba yao kufariki watoto hao hubaki katika familia zao za Kiafrika tu. Katika mahusiano ya kawaida suala la kubaguana lipo baina ya jamii mbili hizo. Adam Shafi katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute* anaonesha kwa Mhindi kujichanganya na Mswahili ni kwenda kinyume na utamaduni wa Wahindi anaeleza:

Jamatini watu ote nazungumza habari yako, nasema veve siku hizi nafatana na golo. Toka! Toka Kwenda zako! Mimi sitaki ona hata uso yako. Kuranjiso, kama veve nakuja tena hapa mimi taita askari, tasemaveve miji nataka iba. Muhuni ve, mwenaharamu, toka! (uk. 43).

Utafiti uliofanyika umebaini kuwa lugha hiyo inatokana na kuendeleza matabaka. Mama yake Yasmin anashindwa kuzungumza Kiswahili vizuri, bila shaka hali hii inasababishwa na tabia yake ya kujitenga na Waswahili. Wahindi wengi ni wafanyabiashara na wanawake hutumika katika kusaidia kazi hizo. Hivyo, Kiswahili kichafu anachozungumza ni kwa ajili ya mawasiliano tu na wateja ambao Waswahili ni miongoni mwao. Wahindi wanajitenga na Waswahili hata hivyo, ndio washitiri wa bidhaa zao. Lugha inayotumika katika dondoo inawakilisha vizuri kundi hilo la utamaduni linaloendeleza utabaka. Hisia za hali ya ghadhabu zinazowasilishwa na mama kumfukuza mtoto wake wa kumzaa hazifai. Ni heri mama huyu angelizungumza na mwanawe kwa hekima na kumpa miongozo ya kuishi hata kama anakwenda kuishi Uswahilini kuliko kumfokea na kumfukuza. Kwa sababu amejitenga na Waswahili mama Yasmin haelewi kuwa “mtoto hanyei kiganja ukakikata”. Matokeo yake Yasmin ameishi maisha ya kihuni kwa sababu hakuwa na namna nyingine kutokana na mfumo wa utabaka uliotamalaki katika jamii yake.

Njogu na Wafula (2007) wanafafanua kwamba Maxim Gorky ambaye ni miongoni mwa waanzilishi wa Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa anaona kuwa ni jambo la kuhuzunisha kwa mtu yule yule amezaa na kuendeleza dhuluma dhidi ya mtu mwenzake. Wanaendelea kufafanua kuwa yeye pamoja na kwamba yu katikati ya idhilali na dhuluma hizi, ana shauku kubwa ya kupinga na kutupilia mbali mateso ya aina yoyote. Hivyo, inahuzunisha kuona mama mzazi anamfukuza mtoto wake kwa kuendeleza dhuluma zinazotokana na utabaka. Kitendo cha mama kumfukuza mtoto wake wa kumzaa ni unyama na kumdhulumu. Hata hivyo, Yasmini mbali na kuwa anakabiliwa na idhilali na dhuluma zinazotokana na utabaka yuko tayari kutupilia mbali mtazamo wa jamii yake ili aondokane na mateso anaeleza:

Ah, haidhuru nitaishihivyo hivyo, yaache maji yafuate mkondo na upepo, uvume utakapo kwani wangapi duniani wenye dhiki. Mwisho wa dhiki si dhiki ni faraja tu, ... Sasa sina mwingine ila mimi na Waafrika, n`do baba zangu, n`do mama zangu, n`do shoga zangu, n`do ndugu zangu. Na wanawadharau kwa sababu gani hasa? Wao si watu? Au kwa sababu masikini? Ikiwa wao masikini basi na mimi nishakuwa masikini, nakula fadhila zao, nakula fadhila za Mwajuma na laiti ingelikuwa si yeye sijui ningeishi vipi mpaka leo. Ah! Haidhuru na waseme wasemayo, potelea mbali (uk.43).

Mawazo hayo katika dondoo yanatoa picha kuonesha kwa kiasi gani Yasmin anaona kuwa jamii yake ina mtazamo usiofaa juu ya Waafrika. Anaona wale wanaodharauliwa na jamii yake ndio hao wanaomfaa. Aidha, katika dondoo hilo falsafa ya Kiafrika ya kusaidiana inajichomoza kwa uwazi. Chuachua (2016) anaonesha kuwa kusaidiana ni miongoni mwa wajibu unaotawala maisha ya Wabantu. Mwajuma ambaye ni Mwafrika na ni Mbantu anawakilisha vyema wajibu huo kupitia riwaya ya *Vuta n`Kuvute*. Waafrika kusaidiana ndio utamaduni unaowaongoza kama mwenzio amefikwa na matatizo unatoa msaada. Tunapozingatia muhimili katika Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa unaoeleza binadamu huoneshwa kiuyakinifu. Wahusika ambao huelezwa kama vipaza – sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao (Njogu na Wafula, 2007, uk. 68). Muhimili huu unatupa nafasi ya kumuona mama Yasmin anavyotumiwa kuwakilisha uhalisi wa jamii ya Wahindi ndani ya Zanzibar wakati wa ukoloni. Aidha, tunamuona Yasmin anavyotumiwa kama kipaza sauti katika kuikosoa jamii ya Wahindi kujitenga na Waafrika. Watu wa taifa moja huishi kama ndugu na kusaidiana pale inapobidi. Hapo ndipo nchi inapoweza kujivunia rasilimali watu wake katika ujenzi wa taifa lao kwa pamoja.

Katika kuonesha namna matabaka yalivyochukuwa nafasi katika jamii ya Wahindi Adam Shafi anaonesha kuwa ni ajabu kubwa kwa mtoto wa Kihindi kufuatana na Mwafrika. Mwandishi huyo anatueleza:

Njiani mote humo Yasmin hakuwa akitembea kwa uhuru kwani mara kwa mara ilibidi ajifiche kila anapokutana na jamaa zake. ... Baada ya matembezi yao walirejea nyumbani (uk. 34).

Mawazo yanayojitokeza hapo ni kuwa dhana ya matabaka humnyima mtu raha ya lolote analolifanya. Yasmin anakosa uhuru katika matembezi kwa sababu jamii yake haimkubali Mwafrika kama mtu wa kuchanganyika naye. Keshodkar (2010: 235) anaeleza kuwa Wahindi wa kike wanapotoka kwenda matembezi hufuatana na familia zao. Hii hufanywa makusudi ili wanawake hao kutokuwa na maingiliano na Waswahili. Hivyo, Adam Shafi kwa namna anavyosawiri muono wa Wahindi juu ya Waswahili katika riwaya na maandiko yasiyo ya kubuni yanavyoeleza. Tunaona kuwa mwandishi

huyo anaisawiri jamii ya Kihindi katika uhalisi wake kama muhimili wa Uhalisia wa Kijamaa unavyotaka wa binadamu kuoneshwa katika uyaikinifu. Adam Shafi anamsawiri binadamu huyo katika uyaikinifu wake.

Matabaka ya kiutamaduni pia yanadhihirika katika matumizi ya kumbi za starehe katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute*. Mwandishi anaonesha kuwa watawala walikuwa na kumbi zao maalumu ambazo Waafrika hawakuruhusiwa kuingia. Mwandishi anaeleza:

Leo tumedhamiria kwenda Karimjee Club. Huseni alicheka sana na kusema, tokea lini Karimjee Club wakaingia watu kama nyinyi? Kwani hamjui kwamba nyumba ile ni ya watukufu tu?. N`do maana tumetia vitu vyote tuonekane kama hao wanaokubalika huko. ... Ulikuwa mkusanyiko wa Wazungu watupu kwani ilikuwa marufuku kwa asiye mzungu kuingia ndani ya klabu ile. Waafrika walioruhusiwa kuingia ndani ya jengo hilo ilikuwa ni wahudumu tu ambao waliwahudumia wazungu wale kwa heshima na taadhima na kuwatetemeka (kur.131 - 149).

Kwa mujibu wa dondoo hilo matabaka yalikuwapo hata katika masuala yanayohusisha starehe na burudani. Watu wengi hufurahia burudani kwa ajili ya kujistarehesha, ni sehemu ya kupumzika na kukonga nyoyo. Watawala walikuwa wanaona hawataweza kufurahi wakiwa pamoja na Waafrika; kwani, kwao hawa hawakuwa na hadhi ya kupata starehe kama wanayoipata wao. Mawazo tunayoyapata kutoka katika dondoo ni kuwa watawala waliwaona Waafrika watu wakati wa mahitaji yao tu. Waafrika waliowahitaji ni wale watumishi wanaowahitaji kwa kuwatumikia. Uhalisi wa matabaka unakwenda sambamba na muhimili wa Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa unaoeleza kuwa binadamu huoneshwa kiuyakinifu. Wahusika ambao huelezwa kama vipaza – sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao (Njogu na Wafula, 2007, uk. 68). Hii ni kwa sababu muhimili huo unatupa nafasi ya kuuona uhalisi wa matabaka wakati wa ukoloni Zanzibar; kwani, Waafrika waliwekwa kuwa ni watu wa tabaka la chini wasiokuwa na hadhi ya kufaidi starehe pamoja na watawala. Ismail (2019) anaeleza kuwa wakoloni walipokuja Afrika waliunda matabaka ya mabwana na watumwa. Hivyo, kwao wao Waafrika wale waliowaruhusu kuingia katika kumbi zao za starehe ni watumwa tu wa kuwatumikia wao kama dondoo lilivyobainisha hapo juu.

Reinwald (2006) anaeleza kuwa Zanzibar wakati wa utawala wa Uingereza kulikuwa na kumbi za sinema kama vile; *Zanzibar Cinema/White Tent* – Mnazi Mmoja, *Merry Theatre/Alexandra Cinema* – Mkunazini, *Royal Cinema* – Vuga na *Sultana Cinema* – Forodhani. Anafafanua kwamba kumbi hizi ziliendeshwa kitabaka wahudhuriaji wa sinema katika kumbi hizi walikuwa Waingereza na marafiki zao wa karibu. Aidha, askari ambao ni Waafrika waliruhusiwa na walitakiwa kulipa nusu kiingilio. Riwaya ya *Vuta n`Kuvute* inaonesha kuwa watawala walijenga dharau kwa Waafrika ijapokuwa walikuwa wakiwaajiri katika nafasi za chini. Wafanyakazi hawa hawakuwa wakitunziwa heshima kama wafanyakazi. Matusi na vipigo viliwaandama wafanyakazi hawa. Dondoo lifuatalo linathibitisha:

Hapana jua, get Out of my office!. Inspekta Wright aliwafukuza na kuwarushia mateke. Askari wale walitimka mbio kila mmoja akakimbia upande wake... Baada ya muda mrefu akiwa ameshughulika na makaratasi yale, aliita kwa kelele “Matata! Matata!” “Afandi!” Kopto Matata aliitika, anakuja mbio. ... “Youidiot” Inspekta Wright alipiga kelele na kuipiga meza ngumi (kur. 148 - 151).

Kinachodhihirika katika dondoo hilo ni dharau. Waingereza waliwadharau wafanyakazi wao. Wengi wa askari hao wa nafasi za chini walikuwa ni Waafrika, waliwaona kuwa ni watu wasiostahili heshima. Nidhamu kwa waajiriwa hao haikuwapo. Waafrika walikuwa hawana thamani hata kidogo mbele ya watawala hao wa kigeni. Hii ni kwa sababu ya rangi yao nyeupe. Kelele anazopigiwa Koplo Matata na Inspekta *Wright* na unyenyekavu anaouonesha askari huyo ndivyo ilivyokuwa inatakiwa na Waingereza. Mghanga (h.t) anaeleza kuwa katika mfumo wa kibepari mtu haheshimiwi kutokana na utu wake au uzalendo wake bali kutokana na pesa. Kwa kuwa Waafrika wakati wa ukoloni hawakuwa na kitu hiyo ndiyo iliyokuwa hadhi yao, ya kutokuthaminiwa. Hivyo, kipigo na manyanyaso viliwakabili wafanyakazi hao wa Kiafrika.

Kwa jumla, Adam Shafi anavyosawiri matabaka yaa kiutamaduni katika *Vuta n`Kuvute*, na utafiti uliofanyika kupitia uchambuzi katika kazi ambazo si za ubunifu kama vile; Reinwald (2006), Keshodkar (2010), Burton (2013), Rustamkhanli (2016), Wahabi (2022) zinaonesha bayana kuwa mwandishi wa riwaya teule anauwasilisha mfumo halisi wa jamii ya Zanzibar wakati wa ukoloni. Katika muktadha huu mawazo ya Ambuyo na wenziwe (2020) yanayoeleza kuwa fasihi humulika tamaduni katika eneo husika na kuwasilisha kisanaa yanabainika moja kwa moja kupitia riwaya hiyo.

4.4 Uhalisi wa Matabaka ya Kijamii

Katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute* matabaka ya kijamii yanabainika kupitia masuala ya elimu na maeneo ya makaazi. Riwaya inaonesha kuwa elimu kwa watoto wa kike haikutiliwa maanani. Denge, Mambo, Mwajuma na Yasmin ni vijana wa rika moja. Denge anaoneshwa kuwa amesoma hadi chuo kikuu, Mambo amesoma na kupata ajira katika Serikali ya Kikoloni. Hata hivyo, riwaya haisawiri tukio lolote kuwa Mwajuma alipata elimu. Aidha, riwaya hiyo inamsawiri Yasmin kuwa alipofikisha umri wa miaka kumi na tano aliozwa mume. Umri huu tunamtazamia kuwa bado angelikuwa anaendelea na masomo yake. Mwandishi wa makala hii anaona mtunzi wa riwaya husika amewasawiri Mwajuma na Yasmin katika hali hiyo kwa sababu ya mfumo wa utabaka uliokuwapo katika jamii. Elimu kwa watoto wa kike haikupelewa kipaumbele. Hivyo, vijana hao wa kike walikosa elimu kwa sababu ya utabaka wa kielimu uliokuwapo wakati huo. Wahabi (2022) anafafanua kwamba elimu kwa mtoto wa kike Zanzibar ilikuwa ni changamoto. Mtaalamu huyo anaendelea kuweka wazi kuwa wazazi wengi hasa wanaofuata dini ya Kiislamu walikataa kuwapatia elimu watoto wa kike.

Kwa upande wa maeneo ya makaazi riwaya inawasawiri Denge, Mwajuma na Waswahili wengine wanaishi Ng`ambo. Eneo la Ng`ambo lilijulikana kuwa ni mitaa duni ya watu masikini wasio na pato (A.S.P, 1977; Khatib, 1992). Hawa wengi wao ni Waswahili ambao walijulikana kuwa ni wenyeji wa Zanzibar. Aidha, riwaya inamuonesha mama Yasmin anaishi Kiponda na Kermali Mchambawima. Hii ni mitaa inayopatikana katika Mji Mkongwe wa Zanzibar. Folkers (2014) anafafanua kuwa Mji Mkongwe ulikuwa ni makaazi ya Wazungu, Waarabu, na Wahindi, mitaa ya Ng`ambo ilikuwa ni sehemu ya wenyeji.

Uhalisi wa matabaka unaosawiriwa katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute* unakwenda sawia na muhimili wa Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa unaoeleza kuwa binadamu huoneshwa kiuyakinifu. Wahusika ambao huelezwa kama vipaza – sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao (Njogu na Wafula, 2007, uk. 68). Suala la matabaka linavyojitokeza katika kazi ambazo si za ubunifu linasawiriwa kiyakinifu katika riwaya

teule. Yale ambayo mwandishi wa makala hii ameyachambua katika kazi kama vile A.S.P (1977), Khatib (1992) na Folkers (2014) yanajitokeza vilivyo katika riwaya iliyotafitiwa.

5.0 Hitimisho

Kwa jumla, makala hii ililenga kubainisha uhalisi wa matabaka unaosawiriwa katika riwaya ya *Vuta n`Kuvute*. Makala imebainisha kuwa mwandishi wa riwaya hiyo anauswiri uhalisi wa matabaka ndani ya jamii ya Zanzibar wakati wa ukoloni katika namna ambayo inaakisi maisha halisi ya jamii ya wakati huo. Matabaka ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii anayoyasawiri Adam Shafi uyanaakisi uhalisi wa maisha kwa jamii husika. Hivyo, *Vuta n`Kuvute* ni zao la jamii inayoonesha kuwapo kwa jamii hiyo katika nyanja tofauti za kimaisha. Riwaya hii ni kioo kinachoonesha jinsi maisha yalivyokuwa Zanzibar wakati wa ukoloni. Aidha, riwaya teule inadhihirisha jiunsi fasihi na historia zinavyotegemeana na kukamilishana. Hali hii inaonesha namna riwaya husika inavyoweza kuwa nyenzo ya kujifunzia historia halisi ya jamii ya Zanzibar wakati wa utawala wa Uingereza. Kwa namna Adam Shafi alivyotumia mwanda, wakati na viwango vya uhalisi amefanikiwa kuonesha uhalisi wa matabaka katika jamii ya Zanzibar wakati wa utawala wa Uingereza.

MAREJELEO

- Adam, O. A. (2014), "Kuchunguza Dhamira za Kiutamaduni na Kijamii katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka *Kuli na Vuta n'Kuvute*", Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa), Iliyosomwa tarehe 10/02/2021 katika <https://www.academia.edu>.
- Almeida, J. F. Machado, F. L. & Costa, A. F. (2006), "Social Classes and Values in Europe", *Portugese Journal of Social Sciences*, 5 (2), 95-117, Iliyosomwa tarehe 2/08/2019 katika www.researchgate.
- Ambuyo, B. A. Makokha, R. & Oketch, S. E. (2020), Mifumo ya Kijamii katika Tamthilia Teule za Kiswahili, *East African Journals of Swahili Studies*, 2 (1), 8-18 Iliyosomwa tarehe 18/02/2022, <https://doi.org/10.37284cajas.2.1.135>.
- ASP. (1977), *Short History of Zanzibar*, Printing Press Corporation.
- Bakari, M. (2011), Racial Identities, Nationalism and the Politics of Exclusion in Zanzibar, *The African Review*, 38 (1&2), 1-35, Iliyosomwa 04/08/2023, journals.udsm.ac.tz.
- Batholomayo, J. I. (2019), "Kuchunguza Siasa na Itikadi katika Tamthiliya ya *Nyota ya TomMboya*" Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa), Iliyosomwa tarehe 13/02/2023 katika repository.out.ac.tz.
- Burton, E. (2013), "The Indian Diaspora, the State and Nation in Tanzania Sinceca. 1850", *Vienna Journal of African Studies*, 13 (25), 1-28, Iliyosomwa tarehe 08/08/2019 katika <https://stich.proben.univie.ac>.
- Chuachua, R. (2016), "Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Mukadha wa Epistemolojia ya Kibantu", Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa), Iliyosomwa tarehe 17/02/2023 katika repository.udom.ac.tz › handle.
- Davine, J. D. (1973). *Case Study of Revolution Zanzibar and Tanganyika Compared*. Ripoti ya Tasnifu Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Arizona, repository.arizona.edu › handle.
- Diegner, L. (2011), "Mazungumzo na Adam Shafi Uandishi Wake wa Riwaya", Iliyosomwa tarehe 10/08/2019 katika www.qucosa.de/fileadmin/data/qucos.documents/9837/18ShafiDiegner.pdf.
- Edward R. (1997), *Modern Britain: A Social History*, London. Arnold.
- Emhemmd, J. A. (2017), "Kuchunguza Dhamira katika Riwaya ya Kiu", Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa), Iliyosomwa tarehe 10/08/2022, repository.out.ac.tz ›
- Enon, J. C. (1998), *Educational Research, Statistics and Measurement*, Kampala, Makerere University.
- Folkers, A. S. (2014). Planing and Replaning Ng`ambo – Zanzibar, *SAJAH*, 29 (1), 39-53, Iliyosomwa tarehe 17/08/2023 katika www.fbwarehitecten.nl.
- Gathenya, E. W. (2018), "Mielekeo na Mtindo wa Shafi Adam Shafi katika Riwaya za *Kuli na Haini*", Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa), Iliyosomwa tarehe 28/01/2021 katika ir.library.ku.ac.ke.

- Haji, G. A. (2015), "Upande wa Pili wa Riwaya Teule za Shafi Adam Shafi: Dhamira zilofichama", Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Dodoma (Haijachapishwa), Iliyosomwa tarehe 22/12/ 2020 katika repository.udom.ac.tz.
- Haji, M. (2018), "Uhalisia wa Utabaka katika Tamthiliya ya Janga la Werevu na Kitumbua Kimeingia Mchanga", Ripoti ya Tasnifu Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu SUZA.
- Institute of Education. (1981), *Development of African Societies upto the Nineteenth Century*, Dar es Salaam, Dar es Salaam University Press.
- Ismail, F. H. (2019), "Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya ya *Mondlane na Samora*", Ripoti ya Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria (Haijachapishwa), Iliyosomwa tarehe 10/ 08/2023, repository.out.ac.tz.
- Kavoi, J. M (2020), "Ukamilifu na Utimilifu wa Kifasihi katika Maandishi ya Kubuni: Mfano wa Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed", *Mwanga wa Lugha*, 5 (1), 139-156, Iliyosomwa tarehe 27/02/2023, <http://ir.mu.ac.ke>.
- Keshodkar, (2010), "Marriage as the Mean to Preserve 'Asian-ness': The Post-Revolutionary Experience of the Asians of Zanzibar", *Journal of Asian and African Studies*, 45 (2), 226-240, Iliyosomwa tarehe 09/08/2019, cite seerx.ist.psu.edu > viewdoc.
- Khatib, M. S. (1992), *Taarab Zanzibar*, Dar es Salaam, Tanzania Publishing House.
- Kuhn, R. (2004), "Class and struggle in Australia: an introduction", Iliyosomwa tarehe 09/08/2019 katika sa.org.au > csaseminars > Class...
- Loimeier, R. (2018), "India Beyond India: The Indian Diaspora in East Africa", *Göttingen Series in Social and Cultural Anthropology*, 12, 151-172, Iliyosomwa tarehe 08/08/2023, katika Doi: 10.1787/gup2020-1268.
- Mapara, J. (2007), "Analysis of the Reliability and Validity of the Shona Novels as a Historical Document, Ripoti ya Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Afrika Kusini, (Haijachapishwa), Iliyosomwa tarehe 28/01/2021, uir.unisa.ac.za > handle > thesis.
- Mapuri, O. R. (1996), *The 1964 Revolution: Achievements and Prospects*, Dar es Salaam, TEMA Publishers Company Ltd.
- Marks, K. & Engels, F. (1845), *The German Ideology*, Iliyosomwa tarehe 15/10/2022 katika www.qualityresearchinternational.com.
- Mbatiah, M. (2016), *Riwaya ya Kiswahili Chimbuko na Maendeleo Yake*, Jomo Kenyatta Foundation.
- Mghanga, M. (h.t), Uhuru na Haki za Binadamu, *Makala ya Mjadala wa Falsafa ya Mapinduzi*. 1 – 40, www.comunistpartyofkenya.org.
- Mulokozi, M. M. (2017), *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuu Vikuu*, KAUTTU, Dares Salaam.
- Njogu na Chimera (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. & Wafula, R. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi
- Ponera, A. S (2019), *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*, Central Tanganyika Press, Dodoma.

- Reinwald, B. (2006), "Tonight at the Empire Cinema and Urbanity in Zanzibar, 1920s to 1960s" *Afrique & histoire*, 5 (1), 81-109, Iliyosomwa tarehe 10/08/2019, <https://www.cairn.info>.
- Rodney, W. (1973), *How Europe Underdeveloped Africa*, Iliyosomwa tarehe 05/08/2019 katika abahlali.org › files › 32953.
- Rustamkhanli, Tengiz (2016), Indian Marriage, 1-4, katika <https://www.academia.edu>.
- Sengo, T. S. Y. M. (1987), *Fasishi Simulizi, Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam, Nyanza Publications Agency.
- Senkoro, F. E. M. K. (1995), "Sanaa, Ubunifu na Jamii katika Nadharia ya Fasihi", *Kioo cha lugha*, 1 (2), 81-92, Iliyosomwa tarehe 04/08/2020, journals.udsm.ac.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011), *Fasihi*, KAUTTU, Dar es Salaam.
- Shafi, A. S. (1999), *VUTA N'KUVUTE*, Dar es Salaam, Mkuki na Nyota Publishers.
- Sheriff, A. (2001), "Race and Class in Politics of Zanzibar", *Africa Spectrum*, 36 (3), 301-318, Iliyosomwa tarehe 07/08/2019 katika www.arts.ualberta.ca › Hist 1347.
- Speller, I. (2007), African Cuba? Britain and the Zanzibar revolution, 1964, *The Journal of Imperial and Commonwealth History*, 2 (35), 283-301, Iliyopitiwa tarehe 10/04/2023, katika warwick.ac.uk › programme.
- Wahab, S. O. (2022), History of Indians in Zanzibar from the 1870s to 1963, Ripoti ya Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Göttingen (Haijachapishwa), Iliyosomwa tarehe 17/08/2023 katika <http://dnb.dnb.de>.
- Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi, Phoenix.
- Wamitila, K. W. (2003), *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*, Kenya, Focus Publication Ltd.
- Wamitila, K. W. (2008), *Kanzi ya Fasihi, Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi, Muwa Publishers.
- Wamitila, K. W. (2008), *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Muwa Publishers.
- Williams, A. -Y. I. (2003), "On the Subject of Kings and Queen: Traditional African Leadership and the Diaspora Imagination", *JOUR*, 7, 59-67, Iliyosomwa tarehe 05/08/2019 katika www.asq.afrcu.ufl.edu.
- Wilson, A. (2007), "Abdul Rahman Mohamed Babu: Politician, Scholar and Revolutionary", *The Journal of Pan African Studies*, 1 (9), 8-25, Iliyosomwa tarehe 07/08/2019 katika jpanafrican.org › docs › Abd.